

6. Huduma za meno

Huduma za meno, katika jimbo la Queensland, hutolewa na idara ya meno ya Queensland ya umma (public) bila ya malipo pamoja na madaktari wa kibinafsi (private). Kuweza kustahiki huduma za bure ambazo zina masharti makali, lazima uwe na kadi ya Medicare, kadi ya pensheni au/na kadi ya watu wazima. Unapaswa pia kuwa mkazi wa Queensland.

Huduma za meno kwa umma

- Afya ya Queensland ina kliniki 520 za meno za umma. Ili kupata kliniki ya meno kwa umma iliyo karibu nawe angalia chini ya afya ya Queensland, (Queensland Health, Dental (oral) Health Services) Huduma ya Afya ya Meno (kinyua) katika kurasa nyeupe za saraka. Kama sivyo, unaweza piga simu kwa laini ya 13 HEALTH nambari ya simu 13 43 25 84
- Kliniki nyingi zina muda mrefu wa kusubiri matibabu ya kawaida ya meno. Katika maeneo mengine muda wa kusubiri ni zaidi ya miaka mitatu.

Huduma za watu wazima – kliniki za bure za meno za umma

- Watu wazima na wanaowategemea ambao wana mojawapo ya kadi zifuatazo zinazotolewa na Centrelink wanaweza kutumia kliniki hizi bila malipo:
 - Kadi ya Pensheni
 - Kadi ya Medicare
 - Kadi ya Pensheni– inayotolewa na Idara ya mambo ya wazee wa jeshi
 - Kadi ya Queensland ya Watu Wazima
 - Kadi ya Afya ya watu wazima wa Jumuiya ya madola
- Kama huna mojawapo ya kadi hizi, unapaswa kwenda kwa daktari wa meno wa kibinafsi.

Huduma za meno zinazotolewa shuleni

- Watoto wote wakazi wa Queensland wenye umri wa miaka min'ne au zaidi ambao hawajakamilisha darasa la kumi shuleni wanastahiki huduma ya daktari wa meno wa umma bila malipo. Huduma hii inapatikana kwa wote bila ya kujali mapato yao.
- Matibabu ya meno ambayo sio ya dharura inapeanwa shuleni kupitia kliniki zilizowekwa au kliniki zitembeazo kwa gari (gari litumiwalo kwa huduma ya meno). Matibabu hayo hutolewa kwa njia ya kutembelea shule moja baada ya nyengine. Toleo la matibabu ya meno hufanywa kwa kutuma fomu nyumbani ili kuidhinisha matibabu.
- Fomu za kutoa ruhusa hupewa wanafunzi wote walioandikishwa shuleni wakati huduma inapoanzishwa shuleni katika kila shule
- Wakati kliniki ya shule imefungwa au haipatikani, mpeleke mtoto wako kwa kliniki ya meno iliyo karibu kwa matibabu ya dharura ya meno.

Daktari wa meno wa kibinafsi

- Unapomuona daktari wa meno wa kibinafsi, lazima ulipie huduma hiyo. Madaktari wa meno wanaofanya kazi kibinafsi wanaweza kupatikana katika maeneo mengi kila pahali Queensland kama vile maeneo ya mitaa na vituo vya ununuzi
- Ili kupata daktari wa kibinafsi unaweza kuangalia katika kurasa za manjano ya saraka ya simu chini ya 'daktari wa meno au Dentist'
- Kama una bima ya afya ya kibinafsi unapaswa kuangalia kama bima yako inatoa huduma ya meno. Hata kama bima yako inatoa matibabu ya meno, inawezana kua haisimamii gharama ya ada zote.
- Kabla kufanyiwa kazi kubwa ya meno, ni vizuri kumuuliza daktari wa meno akundikie takalifu ya kazi hiyo.

Matibabu ya meno ya dharura

- Dharura ya meno ni hali ambayo inahusisha hatari ya moja kwa moja kwa afya ya mtu pamoja na jeraha la dhiki kwa meno au uso, uvujaji wa damu nyingi na kuvimba uso
- Kila Wilaya ya Huduma ya Afya ina utaratibu wake wa dharura ya meno, na watu kwa jumla huchunguzwa kulingana na mahitaji.